Furaha (Claire Watt)
Darasa la Kiswahili
Insha Yangu

# "Maji Usiyoyafika Hujui Wingi Wake":
# Safari Yangu ya Arusha

Kiangazi kilichopita, nilikuwa na bahati kama mtende kuweza kusafiri nchi ya Tanzania kwa muda wa miezi miwili. Kabla ya kwenda Tanzania, nilitaka kuzuru huko kwa muda mrefu sana. Muhula wa kipupwe, nilikata shauri kwamba nitazuru nchi za Afrika ya Mashariki kupitia kwa chama cha kujitolea. Chama hiki kinaitwa "Wanafunzi kwa Badiliko ya Kimataifa" au, kwa Kiingereza, "Students for International Change (SIC)." Wakati nilijua kuwa nitasafiri Tanzania, nilianza kusoma lugha ya Kiswahili. Watu wengi sana ambao wanatoka eneo la Afrika ya Mashariki wanakisema Kiswahili, kwa hivyo nilitaka kujifunza kabla ya kwenda Tanzania. Nilihofia kidogo, kwa sababu sikufikiri kwamba ningeweza kuzungumza na watanzania kijijini. Hasa, ninafikiri kuwa ningeishi na familia ya Watanzania, na nilitaka kuweza kuzungumza na baba, mama na ndugu wale wapya. Huko, nilisoma Kiswahili, nilisoma kuhusu ukimwi na virusi vya ukimwi pia. Nilisoma kuhusu ukimwi kwa sababu lengo kuu la safari yangu ni kufundisha kuhusu ukimwi na uambukizaji wa virusi vya ukimwi.

Mnamo mwezi wa saba, niliondoka mji wa Seattle, ambapo familia yangu inaishi, na nilisafiri hadi uwanja wa ndege wa Kilimanjaro kwa ndege. Kwa sababu ilikuwa mara ya kwanzaa kusafiri Afrika, sikujua cha kutaraji. Hapa, katika uwanja wa ndege, nilijumuika na wanafunzi wengine ambao wanasoma katika chuo kikuu cha Stanford. Tulisafiri pamoja hadi mji wa Arusha kwa basi. Safari haikuwa si ndefu sana, na tulifika mjini baada ya kusafiria basi kwa saa moja. Mji wa Arusha ni wenye vumbi na una kelele mbalimbali. Hata ingawa, niliupenda sana halahala. Nilipenda kusema lugha ya Kiswahili wakati wa kununua parachichi, ndizi, mananasi, maembe, na matunda mengine. Nilipenda kupatana katika soko la Kilombero pia, ambapo niliweza kununua kanga na vitenge vingi vizuri. Siku yangu ya kwanza, sikuweza kupatana. Kwa mfano, nililipa elfu tisa kanga moja, lakini nilihitaji kulipa elfu mbili au elfu tatu tu! Lakini, baada ya wiki moja, nilijifunza sana kuhusu masoko na mji kwa jumla.

Halafu, niliaga mji wa Arusha, ambapo nilikaa hoteli rahisi sana, na nilikwenda kijijini. Kijiji changu (ambapo niliishi kwa wiki saba) kinaitwa Siwandeti, na kiko katika mlima wa Meru. Si mbali sana na barabara kuu kwa gari, lakini ni mbali kwa miguu! Kijiji hiki kina mashamba mengi ya ndizi na buni ya kijani. Nilikaa na familia ya Wamaasai. Baba yangu anaitwa Aron Mollel, na yeye ni mzee wa baraza la Siwandeti. Alipenda sana kunisaili maswali mengi kuhusu mimi, na masomo, na familia yangu huko, na Marekani kwa jumla. Hajawahi kutembelea Marekani, kwa hivyo alitaka kujua vitu vingi sana kuhusu nchi ya Marekani.

Nilipenda kuzungumza na yeye pia, na kumsaili maswali mengi kuhusu kazi yake, familia yake, na utamaduni wa Wamaasai. Mama yangu anaitwa Omega Mollel, au Mama Glady. Mama Glady alikuwa na kazi nyingi sana! Huamka kila siku saa kumi na moja alfajiri, kuanza kupika chamshakinywa. Alinifundisha kupika chai na maji, maziwa, majani, na sukari. Mama Glady alipenda kucheka sana, hasa wakati nilijaribu kusema Kiswahili.

Nilikuwa na ndugu wanne – dada yangu Gladness ana miaka kumi na miwili, dada yangu Sayuni ana miaka kumi, kaka yangu Abedinego ana miaka minane, na dada yangu mdogo anayeitwa Faraja, ana miezi mitatu tu! Dada Glady alikuwa mkali sana, kwa hivyo yeye ni mwanafunzi mzuri sana. Alipenda kuchora sana, na aliumbia mimi sanaa nyingi. Sayuni ni mkali sana pia, lakini yeye hakupenda masomo. Kila ndege huruka na mbawa zake, lakini Sayuni alikuwa bila kifano. Badala ya kusoma, alipenda kucheza kandanda, kuimba, na kucheza densi. Alinifundisha wimbo wa Kiswahili, na tulicheka pamoja sana. Abedinego, kaka yangu, ni mtoto mzuri sana, na hakuwahi kuchoka kunifundisha msamiati wa Kiswahili. Kama watu wanasema, “mwanzo wa chanzo ni chane mbili.” Wakati nilihitaji kuondoka Siwandeti kurudi Marekani, alitaka kuja na mimi kuona nyumbani kwetu Seattle. Faraja, dada yangu mdogo, ni mtoto mchanga. Yeye ni mzuri sana, na ana macho makubwa na majuvi sana.

Wiki hiyo, nilienda katika shule ya msingi kuanza kufundisha juu ya ukimwi na virusi vya ukimwi huko. Nilifundisha katika shule za msingi Olchoki na Natema. Wanafunzi wangu wote ni wakali sana, na walipenda kujibu maswali yangu darasani kuhusu ukimwi. Dada zangu Glady na Sayuni wanasoma katika Olchoki, na nilifundisha madarasa yao. Halafu, baada ya masomo, tulirudi pamoja nyumbani kula ugali na kunywa chai. Kabla ya kulifahamu jina langu, waliniita “mzungu wetu” tu! Sikuweza kufundisha darasa la akina Abedinego pia, kwa sababu yeye ni mdogo sana, lakini ninapenda kucheza kandanda na yeye kila siku baada ya masomo. Niliipenda familia yangu sana, na siwezi kukaa zaidi bila kuwaona tena!

Ninaihamu Tanzania, Siwandeti, na familia ya Watanzania sana. Lakini, penye nia pana njia, na nimefurahi kwa sababu nitarudi Tanzania kiangazi hiki. Nitaenda kufanya kazi kwa Wanafunzi kwa Badiliko ya Kimataifa tena, na nitaishi kijijini karibu na mji wa Arusha kwa muda wa miezi mitatu. Wakati huu, nitaishi na Cheka, rafiki yangu ambaye anasoma Kiswahili darasa la Mwalimu Mohochi pia. Ninaamini sisi tutakuwa na wakati mzuri sana!